



Milele Zanzibar Foundation

Kuongeza Maendeleo, Accelerating Progress



Mbweni - Zanzibar: P.O.Box 933

Tel: +255 772 229 997 - +255 777 733 744

info@mzfn.org

www.mzfn.org

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Wizara ya Afya Zanzibar kwa kushirikiana na Milele Zanzibar Foundation inatangaza nafasi za kazi kwa ajili ya vituo vya afya Unguja na Pemba kama ifuatavyo:-

1. DAKTARI WA BINAADAM DARAJA LA II

Nafasi 2 (1 Mtofani na 1 Bumbwisudi)

SIFA ZA WAOMBAJI

- Awe mwenye Shahada ya kwanza katika fani ya Tiba ya Binaadamu (Medical Doctor) kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- Awe amemaliza mafunzo ya vitendo (Internship) kwa muda wa mwaka mmoja katika hospitali zilizoteuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar
- Awe na leseni iliyosajiliwa na Baraza la Madaktari Zanzibar
- Awe na uzoefu wa Kufanya kazi angalao miaka 2
- Awe Mchapakazi, ana mashirikiano mazuri, anaweza kutatua matatizo na anaidhamu ya kazi
- Awe anaishi katika wilaya husika

MAJUKUMU

- i) Kufanya shughuli zote za utibabu, huduma za upasuaji wa dharura na upasuaji wa kawaida.
- ii) Kusimamia wafanyakazi walio chini yake.
- iii) Kusimamia Kituo na kusaidia Kuongeza ubora wa huduma
- iv) Kuchunguza, kufatilia na kuzuia miripuko ya magonjwa mbali.
- v) Kupanga na Kufanya tathmini ya huduma za afya.
- vi) Kuandaa mipango na makisio ya bajeti ya huduma za afya

2. MFAMASIA DARAJA LA III

Nafasi 5; Unguja nafasi 1 na Pemba nafasi 4 (Bumbwini Kiongwe, Sizini, Kangagani, Michenzani na Vikunguni)

SIFA ZA WAOMBAJI

- Awe mwenye Stashahada ya Ufamasia kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- Awe amesajiliwa na Bodi ya Vyakula na Dawa Zanzibar.
- Awe na leseni ya ufamasia
- Awe anaishi wilaya husika

MAJUKUMU

- i) Kuainisha na kutayarisha mahitaji ya mwaka ya dawa na vifaa vyengine vya kitabibu.
- ii) Kutayarisha bajeti kwa ajili ya dawa na vifa vya kitabibu.
- iii) Kufanya manunuzi, kuhifadhi na kuhakiki dawa.
- iv) Kusimamia na kushauri matumizi bora ya dawa.
- iv) Kugawa dawa na vifaa vya kitabibu kwa wagonjwa.
- v) Kutengeneza na kuchanganya dawa.
- vi) Kuandika ripoti za utekelezaji wa kazi ikiwemo ripoti ya robo, nusu na mwaka.

vii) Kusaidia katika kazi nyinyinezo zinazohitajika kwa ajili ya Kuboresha huduma za afya

3. MUUGUZI DARAJA LA III

Nafasi 9; Unguja nafasi 2 na Pemba nafasi 7 (Kiongwe 1, Ukongoroni 1, Sizini 2, Kangagani 2, Michenzani 2 na Vikunguni 1)

SIFA ZA WAOMBAJI

- Awe mwenye Stashahada katika fani ya uuguzi kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- Awe amesajiliwa na Baraza la Wauguzi na Wakunga Zanzibar.
- Awe na leseni ya uuguzi
- Awe anaishi katika wilaya husika

MAJUKUMU

- i) Kutumia utaratibu wa kubainisha mifumo ya Uuguzi na Ukunga (Nursing Process).
- ii) Kutunza vifaa vya kazi.
- iii) Kufanya kazi za kiuguzi za kuhudumia wateja katika jamii, hospitali na sehemu zote zinapotolewa huduma za Afya.
- iv) Kukusanya takwimu muhimu za Afya.
- v) Kuwaelekeza na kusimamia wauguzi na wakunga walio chini yake.
- vi) Kutayarisha mpango wa kazi kwa ajili ya huduma za uuguzi na Ukunga.
- vii) Kutoa huduma za kinga na uzazi
- viii) Kuelimisha wagonjwa na jamii

10. TABIBU (CLINICAL OFFICER) DARAJA LA III

Nafasi 4; Unguja nafasi 2 na Pemba nafasi 2 (Kiongwe 1, Ukongoroni 1, Sizini 1 na Michenzani 1)

SIFA ZA WAOMBAJI

- Awe mwenye elimu ya Stashahada ya utabibu (Clinical Medicine) kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
- Awe na leseni ya Tabibu Kutoka Baraza la Madaktari Zanzibar.
- Awe anaishi katika wilaya husika

MAJUKUMU

- i) Kuchambua na kupanga na kutekeleza huduma za afya ya msingi
- ii) Kutambua na kutibu mgonjwa wa kawaida
- iii) Kuweka kumbukumbu za vifaa na zana za kutolea huduma

JINSI YA KUOMBA

Maombi yote yakiambatanishwa na Barua, Vyeti na CV yatumwe kupitia email hii info@mzfn.org kuanzia tarehe 08 Oktoba, 2022 hadi tarehe 19 Oktoba, 2022.

TANBIHI

Wizara ya afya Zanzibar na Milele Zanzibar Foundation inawatahadharisha waombaji wote kwamba ajira zinatolewa bure. Hivyo, wanatakiwa kujiepusha na Matapeli wanaotumia nafasi hizi kwa kujipatia kipato kisicho cha halali. Watakapo fanikiwa kupata ajira hizi watapewa mkataba wa muda maalumu na wanatarjiwa kuanza kazi tarehe 1 Novemba, 2022.